YAWALETA

MAOMBI

NJIA YA

UZIMA

Mfululizo wa mafunzo katika
Maombi kwa mtu binafsi

YALIYOMO

Kipindi cha 1	***Maombi: Kuwasiliana na Mungu***
Kipindi cha 2	***Kumsikiza Mungu na Kuzungumza Naye***
Kipindi cha 3	***Sala ya Bwana***
Kipindi cha 4	***Kuomba kulingana na Maandiko***
Kipindi cha 5	***Saumu***
Kipindi cha 6	***Kuomba katika Roho***

MAOMBI: KUWASILIANA NA MUNGU

Maombi ni njia ambayo Mungu amempa mtu ili awasiliane Naye. Ni katika kuwasiliana na Mungu, muumini atawezeshwa kuhifadhi uhusiano wake pamoja Naye. Kwa sababu ya uhusiano huo, mtu atajua mapenzi ya Mungu. Katika kutii mapenzi ya Mungu, ndipo tutaweza kuueneza ufalme wa Mungu. Kwa yule anayeamini, maombi yanakuwa njia ya uzima.

1. MAOMBI – UHUSIANO NA MUNGU
Uhusiano pamoja na Mungu unatokana na wakati ambao tunashinda na Mungu.

(a) MIFANO KUTOKA KWA AGANO LA KALE.
Kutokana na uhusiano wao wa karibu na Mungu, **Ibrahimu, Musa** na **Daudi** walimkaribia Mungu. Walimuomba kulingana na uthabiti wa moyo Wake ambayo alikuwa amewafunulia vile alivyo baada ya kuchukua muda wa kukaa Naye. Haja zao na sala zao zilitokana na misingi ya yale waliojua kumhusu Mungu – Asili yake aliyokuwa amewafunulia. **(Mwa.15:6) Ibrahimu** anahesbiwa haki kwa sababu ya imani yake. Alimjua Mungu kuwa Mungu Mwaminifu. Alipofanya maombezi kwa ajili ya Sodoma, alimwambia Mungu, "***Je! Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu?" (Mwa.18:23)***
Ibrahimu aliujua moyo wa Mungu wa kuwaokoa wenye haki na kwa hilo anamuomba Mungu. ***(a.23-32).***
a.25: "Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; Mhukumu ulimwengu wote asitende haki?"

Musa alikuwa amejifunza jinsi ya kutegemea Uwepo wa Mungu katika hali zote. Wana wa Israeli walitambua uhusiano wa ajabu ambao Musa alikuwa nao na Mungu. Walimwona akiingia katika Hema ya mkutano kuzungumza na Mungu. ***(Kut.33:8)***
Wakati Musa alipomlilia Mungu kwa ajili ya Uwepo Wake kuenda nao, alisema, "***Kwa maana itajulikanaje kuwa nimepata neema mbele zako, mimi na watu wako? Siyo kwa sababu unakwenda ansi, hata mimi na watu wako tutengwe na watu wote waliojuu ya uso wan nchi?" (Kut.33:16)*** Musa alikuwa na ujasiri wa kumkumbusha Mungu juu ya Agano Lake kwa Ibrahimu, Isaka na Israeli (***Kut.32:13)*** na kumwambia kuhusu heshima Yake.***(a.12)***

Daudi alichukua muda mwingi na Mungu, akijifunza njia Zake, akijifunza jinsi ya kumtumainia kabisa, na kuishi katika kumwogopa Yeye. Nyingi ya Zaburi ni hoja za Daudi anapoitia uasili wa Mungu kukomboa au kumuokoa.
Zab.56:3-4: "Siku ya hofu yangu nitakutumaini Wewe; kwa msaada wa MUNGU nitalisifu Neno Lake. Nimemtumaini Mungu sitaogopa; Mwenye mwili atanitenda nini?"

(b) YESU ALIFUNDISHA JUU YA MAOMBI
(i) Kama mfano: Yesu alijua umuhimu wa kuwa katika uhusiano na Mungu.
Vile wanafunzi walipokuwa wakichukua wakati Naye, Aliwafunulia na kuwajulisha Vile Mungu alivyo – Asili Wake.
***Yoh. 14:9*: "Aliyeniona Mimi amemwona Baba."**
Yoh. 10:30: "Mimi na Baba tu umoja."
Aliwafundisha wanafunzi Wake kama mfano wakumwomba nani, kuomba lini, jinsi ya kuomba na kwa nini kuomba.
Alimwomba **Nani** katika maombi? ***Luka 11:2***
Aliomba **Wakati** gani? ***Marko 1:35 Luka 6:12***

Yesu aliwafundisha **Jinsi** gani ya kuomba? ***Mt.6:9***
Kwa nini Yesu(Bustani ya Gethsemane) aliwahimiza wanafunzi kuomba? ***Lu. 22:40,46***
Alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake kuwa maisha bila maombi ni maisha yasiyokuwa na mwongozo kutoka kwa Mungu na huongoza katika majaribu na dhambi. [Matt.26:41; Mk.14:38; Lk.22:40 &22:46]
Yakobo 4:2-3 pia anaonya waaminio kuwa *"**hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tama zenu,"***

(ii) Katika mifano: ***Aliwafundisha kuwa na saburi.***
Luka 18:1: *"**Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tamaa."*** Wakati muumini anapoendelea katika kuugua na kudumu katika maombi, Bwana anazalisha kitu.

(c) YESU ALIWAFUNDISHA WAAMINIO:
(i) ***Kuomba kwa imani – wakitarajia majibu.***
Luka 18:8**:** *"**Walakini , atakapokuja Mwana wa Adamu je! Ataiona imani duniani?"***
Yesu aliahidi kuwa ***"ishara hizi zitawafuata waaminio" (Mk16:17),*** na **matarajio Yake ni kwamba waaminio wataomba katika utiifu kwa Bwana wakimwamini kwa ishara.**
Marko 11:24: "Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."
Yohana 15:7: "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."
Yohana 14:13-14: "Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiomba lo lote kwa jina langu, nitalifanya."

(ii) ***Kuomba kwa mamlaka*****: Tunatakikana kujua mamlaka ambayo Kristo ametupatia na tuombe na hakikisho la hayo mamlaka.**
Luka 10:19: "Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakacho wadhuru."

(iii) ***Kumuomba Mungu kwa ujasiri:***
Kwa kifo chake, alimpatanisha muumini na Mungu na kwa hivyo tumepewa uhuru wa kupaingia Patakatifu kwa Baba mbinguni.
Ebr.10:19 *"**Basi, ndugu, kwa kuwa tunaujasiri wa kupaingia Patakatifu kwa damu ya Yesu"***
Ebr. 11:6"Lakini pasipo imani, haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima kwanza aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." **Hizi ahadi zinategemea uhusiano tulionao Naye.**

2. WAAMINIO WATAWEZAJE KUKARIBIA MUNGU KATIKA MAOMBI?
Hebu tuchunguze maandiko yafuatayo ambayo yanatupatia mwongozo wa jinsi ya kumuendea Mungu.
(a) ***NA SHUKRANI***
Zab.100:4: "Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Tu watu wake, nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini Jina Lake."
Kol.1:12-14: "Mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru. Naye alituokoa katika nguvu za giza akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo Lake, ambaye katika Yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi."

(b) ***KATIKA SIFA NA KUMSUJUDIA MUNGU***
Efe.1:3: "Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliye tubariki kwa Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo."
Zab.8:1: "Wewe, MUNGU, Bwana wetu jinsi lilivyo tukufu Jina Lako duniani mwote! Wewe umeuweka utukufu wako mbinguni!"

(c) ***KATIKA KUKIRI***
Tunamwendeaje?
Zab.51:1-2: "Ee Mungu, unirehemu, Sawa sawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu."

Tunamwendea nani?
Ebr.3:1:"Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani wa maungamo yetu, Yesu."

(d) ***KATIKA DUA***
Tunamwendea kwa ujasiri yeye tunayemjia,
1 Yohana 5:14-15: "Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, yakuwa tukiomba kitu sawa sawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kuwa atusikia, tuombacho chote twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."

Na uhakika kuwa yeye ni Mwaminifu.
Fili. 4:6-7 "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."

(e) ***KATIKA MAMLAKA YA KIVITA***
Tunakubali mamlaka ambayo Yesu ametupatia "juu ya nguvu zote za adui". ***(Luka 10:19)***

Tunajua nguvu za Yule tunayemwendea,
2 Kor.10:4: "Kwa maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome."

Na kutumia silaha ambazo ametupatia, tukitambua mamlaka ya Maandiko Matakatifu.
Efe.6:17-18: "Na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho."

(f) ***KWA NIABA YA WENGINE***
Nyaraka za Paulo zinatupatia himizo nyingi za kuwaombea wengine.
Efe.6:18: "Mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote-"
1 Thess.1:2: "Twamshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu nyote, tukiwataja katika maombi yetu."
1 Tim.2:1-2: "Basi kabla ya mambo yote, nataka dua na sala, na maombezi na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu."

(g) ***KULINGANA NA MFANO WA YESU***
Wanafunzi walimuuliza Yesu awafundishe jinsi ya kuomba.**(*Mt.6:6-13*)**
(h) ***BILA KUKOMA***

1 Thess.5:17 "Ombeno bila kukoma."
Roho zetu ziko uhai mbele za Mungu kila wakati. Kuomba bila kukoma, tunakuwa tunamtegemea Roho Mtakatifu wa Mungu. Wakati mwingine hatujui jinsi ya kuomba ama kile tuastahili kuombea. Mungu ameahidi kutusaidia katika hali hii. ***[Rum.8:26]***

(i) *KATIKA NGUVU ZA ROHO MTAKATIFU*
Rum.8:26 "Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi utupasavyo, lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa."

3.NI KITU GANI KINATENDEKA WAKATI TUNAPOSALI?
(a) *ROHO MTAKATIFU ANAWASHUKIA WATU WAKATI WANAOMBA.*
Matendo 4:31:"Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri."

(b) *UPONYAJI HUSHUKA WAKATI WATU WANAPO-OMBA.*
Yakobo 5:15: "Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hataikiwa amefanya dhambi, atasamehewa."
Matendo 28:8:"Ikawa babake Publio alikuwa hawezi homa na kuhara damu. Paulo akaingia kwake, akaomba, akaweka mikono yake juu yake, na kumpoza."

(c) *KUNAFURAHA WAKATI MUNGU ANAPOJIBU MAOMBI.*
Yohana 16:24:"Hata sasa hamkwomba neno kwa jina langu; ombeni nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu."

(d) KANISA LINAKUA.
Wanafunzi wa kwanza walipojitolea ***"kwa maombi na huduma ya Neno"(Matendo 6:4), "Neno la Mungu likaenea, na hesabu ya wanafunzi ikaongezeka Yerusalemu, na wengi wa makuhani wakatii imani" (Matendo 6:7).***

(e) BWANA HUZAWADIA.
Luka 11:9-10: "Nami nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa, Tafuteni, nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa."
Bwana anawaahidi kuwafanyia nini wale ambao wanamjia wakiamini? ***Ebr.11:6***

Na tuombe kwa kuamini na kutarajia.
Yesu alisema "wenye nguvu", yaani, wale wanaojihuzisha na maombi watauteka ufalme kwa nguvu. ***(Matt.11:12)***

Tuombe na mamlaka na tuendeleze utawala wa Mungu hapa duniani.
Yesu ametupatia mamlaka katika maombi "**juu ya nguvu zote za adui, wala hakuna kitu kitakachotudhuru kamwe." (*Luka 10:19)***

ACHA "TUPENYEZE" KATIKA MAOMBI
ILI UFALME WA MUNGU UENEE. (Lu 16:16)

ZOEZI: Soma maandiko haya ili uone jinsi Mungu anavyojibu maombi.

1 Wafalme 18:36-39	**Ayubu 42:10**	**Matendo16:25-34**
1 Wafalme 18:41-46	**Yona 2:1-2&10**	

Ayubu: 42:10 Yona 2:1-2, 10 Matendo16:25-34

KUMSIKIZA MUNGU
na
KUZUNGUMZA NAYE.

Mungu alipomuumba mtu, alimuumba kwa mfano wake na sura yake na kumtuma "atawale nchi yote" ***(Mwa. 1:28).*** **Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu ili aweze kuwasiliana nasi na huu umekuwa mpango wake na haja yake kuelekeza na kuongoza mtu kutimiza mpango huo.**

MUNGU NA MANABII
Mungu ameahidi kwamba hawezi kufanya jambo lolote kabla ya kuwajulisha manabii ***(Amosi 3:7)*** na Biblia imejaa mifano ya Mungu akiwasiliana na mwanadamu, akishirikiana na mwanadamu juu ya kile anataka kufanya. **Mungu bado anataka kunena kwa njia ya manabii kwa kujenga kanisa Lake.** Katika Agano Jipya, mtume Paulo anatukumbusha kwamba Nyumba ya Mungu itajengwa juu ya msingi wa mitume na manabii.***(Efe 2:20)***. Katika Maandiko Matakatifu, Mungu anaendelea kuwahimiza watu Wake kwamba atakuwa nao, kwamba hatawaacha kamwe***.(Kumbu.4:31)***

MUNGU ALINENA NA WATU KAMA RAFIKI
Katika Maandiko tunaona mifano ya wanaume na wanawake wakimsikia Mungu na kunena Naye kama rafiki kwa mfano, ***"Naye BWANA akasema na Musa uso kwa uso, kama vile asemavyo na na rafiki yake" (Kut. 33:11).***

MUNGU ANANENA NA WATU KATIKA YESU KRISTO
Ebr.1:1-2 "Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwiso wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana."

MUNGU ANANENA NA WATU KWA ROHO MTAKATIFU
Wakati Yesu aliporudi mbinguni, aliahidi kutuma Roho Mtakatifu akae nasi. Alituhakikishia Roho mtakatifu atafanya nini?
Yohana 14:26 "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."

Leo hii tunapotafuta kutimiza Tume Kuu, tunaweza kutarajia Mungu kunena nasi na kutuongoza kama jinsi amefanya siku za kale. Yesu aliahidi kujenga kanisa Lake.***(Matt. 16:18)*** Lakini jukumu hilo amewaachia watakatifu kutekeleza, kwa ahadi,*"**Tazama, mimi nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari" (Matt. 28:18-20).***

Tutajuaje mahali pa kwenda na cha kufanya, Bwana asiponena nasi na kutuongoza?

Biblia inawaitaje wale ambao wanaongozwa na Roho wa Mungu? ***Rum 8:14 [wana wa Mungu]*** **tunapomtumaini, Mungu anaahidi kutufanyia nini?** ***Zab.32:8 [fundisha na kuongoza]***

Tunatakikana kumsikiliza Mungu na kuutafuta uso Wake; tukingojea kwa matarajio kuwa atajibu; tukiwa katika uhusiano pamoja Naye katika njia ambayo Roho Mtakatifu atatufunulia "*mambo yanayokuja" (Yoh 16:13).*

Kama marafiki Wake, Yesu atatimiza ahadi Yake kutujulisha yale yote ambayo

amesikia kutoka kwa Baba Yake kwa njia ya Roho Mtakatifu *(Yohana 15:15),* ili kwamba "chochote mtakacho omba Baba katika Jina Langu atawapa" *(a.16).*

MUNGU ANAONGOZAJE?

A) BIBLIA – NENO LA MUNGU.
B) ROHO MTAKATIFU –kwa NDOTO, MAONO na UNABII.
C) MAMBO.

A) BIBLIA – NENO LA MUNGU.
Biblia ni Mungu anena nasi.
***Imeandikwa na watu waliowezeshwa na Roho Mtakatifu*.**
2 Tim.3:16 : "kila Andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."
Rum.15:4 inasema kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi, ***"ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini."***

(a) Neno la Mungu linatuongoza.
Zab.119: 105 "Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu."
Mungu ameahidi kuliweka Neno Lake katika mioyo yetu na sheria Zake katika nia zetu. ***(Yer.31:33)***

(b) Ni mapenzi ya Mungu yaliyoelezwa.
Mungu ameeleza mapenzi Yake katika Neno Lake. Hatuhitaji maelezo mengine jinsi ya kufanya mambo katika sehemu nyingi za maisha yetu. Kwa mfano ***Gal.5:19-21*** **mwongozo wa maadili** na **maonyo kuhusu wale wasio tii.**

(c) Ni waraka wa Mungu kwa mwanadamu. Ni thibitisho la Mungu na mwanadamu. Inaitwa "Neno la Mungu" maana inanukuu njia nyingi ambazo Mungu amenena na mwanadamu. Tangu pale mwanzo katika kitabu cha Mwanzo, tunamuona Mungu akimtafuta mwanadamu[Adamu] ili anene naye. ***(Mwa.3:9)***
Anampa maelezo maalum **Nuhu** "aliyeenda na Mungu" ***(Mwa.6:9),*** na kwa **Abramu**.***(Mwa.12:1-3)*** watu hawa wawili walikuwa watiifu kwa Mungu na kwa sababu hiyo wakabarikiwa.

(d) Inafichua asili ya Mungu. Hili ni la muhimu kwa sababu ni kutokana nasi kujua asili ya Mungu tutajua jinsi ya kunena Naye.

Kuna **mijadala mingi kati ya Mungu na Mwanadamu** ambayo imenukuliwa katika Maandiko. Twasoma kuwa ***"Mungu akasema...."*** *na* ***"Neno la Bwana likamjia..."*** Hata katika kuwakemea Haruni na Miriamu, Bwana aliwaambia kuhusu **Musa**, *"****Kwake nitanena mdomo kwa mdomo, maana waziwazi wala si kwa mafumbo." (Hes.12:8)***
Kwa mfano Mungu alinena na Ibrahimu **(Mwa.18:23-32)**
na Musa **(Kut.33:12-23)**
na Yeremia **(Yer.1:4-8)**
na Anania **(Matendo 9:10-16)**
Hawa pamoja na wengine wengi walijua uthabiti wa moyo wa Mungu maana walichukua wakati wa kukaa Naye. Kwa hivyo, walikuwa na ujasiri wa kunena na Mungu na wakamsikia kikamilifu. Kwa sababu ya uhusiano wao Naye, hawa watu walibadilisha mtindo wa maisha walipowasiliana na Mungu. Maandiko yanawanukuu **wakijitenga na kuwa na wakati pekee yao na Mungu.** Ili uweze kumsikia Mungu

kikamilifu, **sisi, pia, tunahitaji kujitenga tuwe Naye.** Hatutamsikia Mungu kikamilifu ikiwa nusu na kumakinika kwetu kutakuwa katika mambo mengine.

JINSI YA KUELEWA NENO LA MUNGU

Kwa sababu Neno la Mungu lina pumzi ya Mungu, tunahitaji **kumwomba Roho Mtakatifu ufunuo au ufahamu tunaposoma.** Yesu aliahidi kuwa Roho Mtakatifu Atakuja na kutuongoza katika kweli yote. **(Yoh. 16:13)** Mtume Paulo anatuombea ufahamu katika **Efe 1:17-18.** Yesu alisema, *"**Mkikaa ndani ya Neno langu, ninyi ni wanafunzi wangu hakika. Na mtajua ukweli na ukweli utawaweka huru."(Yoh. 8:31-32)***

B) ROHO MTAKATIFU

Roho Mtakatifu anaongoza kwa njia ya Ndoto, Maono na Unabii

Mungu ameahidi mwanadamu ndoto, maono na unabii kwa kuja kwa Roho Wake Mtakatifu.

Yoeli 2:28 "Hata itakuwa baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; Na wana wenu waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono."**Siku ya Pentekoste, unabii wa Yoeli ulitimia.** ***(Matendo 2:17)***

MUNGU ALINENA NA WANADAMU KWA NDOTO MAONO NA UNABII:

(a) Kueleza yanayokuja

Ndoto na maono mara nyingi hutabiri. Yusufu alikuwa na ndoto zake na pia alipewa uwezo wa kutafsiri ndoto za watu wengine ambao Mungu alikuwa amewapa ndoto. ***(Mwa. 37:5, 40:8, 41:15)***

Yesu aliahidi kuwa Roho Mtakatifu atatuonyesha yale yatakayokuja. (Yoh. 16:15) Pia alitwambia *"Mwana hawezi kufanya lo lote, bali kile anaona Baba akifanya, Mwana pia anafanya."(Yoh. 5:19).*

(b) Kuleta maonyo

Mungu alinena na Labani, baba mkwe wa Yakobo katika ndoto. ***(Mwa. 31:24)*** Mungu alimwonya Yusufu na wale Mamajusi watatu katika ndoto. ***(Matt. 2:12-13)***

Kitabu cha Ufunuo kinanukuu maono ambayo Yesu alimpa Yohana. Kitabu kizima kinaonya mwanadamu na pia kimejaa ahidi za ajabu kuhusu mahali aliko Kristo sasa na mahali tutakuwa siku moja.

(c) Kutoa mwongozo na himizo kwa Mungu.

Mithali.29:18 inatwambia kuwa pasipo maono, watu hawana tumaini. Petro aliona maono ambayo yalimwandaa kwenda kwa Mataifa na Injili. ***(Matendo 10:9-16)***

KILE CHA KUFANYA WAKATI UNA NDOTO, MAONO AU UNABII

Tutarajie Mungu kunena katika ndoto, maono na unabii na pia kupitia kwa Neno Lake. Mungu anapotoa ndoto au maono, ni wajibu wetu kumtafuta kwa ajili ya ufahamu wa kile ambacho amefichua. Wakati mwingi kipawa cha kutafsiri hutolewa katika mikutano ya maombi ya pamoja. Wakati mwingine inafaa kutafuta ufahamu wake kutoka kwa mtu wa Mungu anayejulikana kuwa na kipawa cha kupambanua. Kile ambacho kimefunuliwa kitalingana na Maandiko na kutuacha na amani.

Hab.2:1 anatuhimiza ***"kuangalia ili tuone kileatakachotwambia, na jinsi nitakavyo jibu katika habari ya kulalamika kwetu."***

a.2-3 : Bwana anapeana mwongozo wa kuandika maono na kungojea kutimia kwake.

Omba kwa ajili ya maono au ndoto hadi itimie.

AMANI KATIKA ROHO MTAKATIFU
Neno la unabii likitolewa katika mkutano litawahimisa wale walioko, kukosoa kulingana na Maandiko, kuthibitisha kile wasikilizaji wanahisi Mungu kuwa anasema. **Mwongozo wa Mungu kila wakati utakubaliana na Maandiko, na kutuacha na amani.** Mungu haleti kuchanganyikiwa ama mashaka. Roho Mtakatifu anatuongoza wakati ambapo tunaambatana na Mungu. Anatushawishi juu ya dhambi na makosa, lakini yeye hata tuhukumu sisi.

Wakati **Roho Mtakatifu** anavyoshawishi, yeye **wakati wote** huonyesha jinsi ya kusawazisha hiyo hali. **Anarejesha amani yetu**, ila hukumu hutuacha na usumbufu na huonekana kanakwamba hakuna njia ya kuepuka hiyo hali. Hivi ndivyo tunaweza kutofautisha kati ya Ushauri Wake na mashutumu ya shetani.

(C) MAMBO
Kuna nyakati zingine ambapo **Mungu anafungua milango** na anatupatia **nafasi** ya kuendelea na jambo ambalo ametupatia kufanya. Milango hii hufunguka **kwa wakati wa Mungu.** Kwa mfano Petro alipokea maono kutoka kwa Mungu na hakikisho kutoka kwa Roho wa Mungu. [Matendo10:10-16] [Matendo10:19-20]
Thibitisho lilikuja wakati wageni walipowasili na kumwalika kwenda pamoja nao kwa nyumba ya Kornelio. Mlango ulifunguliwa kwake ili atii hayo maono***. (Matendo 10:9-23)***
Mungu anapofungua mlango, hali zetu huambatana na yale ambayo Mungu anasema katika Biblia. Roho Mtakatifu anatupatia amani katika hali ilitujue kuwa ni Mungu anayenena nasi.
Yesu anasema nini kuhusu mlango ule anaoufungua na kufunga? ***Ufu.3:7***

Ili tuwe na uhakika wa kuwa katika mapenzi ya Mungu, haya mambo matatu, Neno la Mungu, uthibitisho wa Roho Mtakatifu anaopeana kwa njia ya Maono, ndoto au unabii, na hali zetu lazima ziambatane na hayo.

NITAWEZAJE KUMSIKIA MUNGU WAZI WAZI?
Tenga wakati wakuwa pamoja naye mahali pasipo na makelele. ***(Marko 1:35)***
Tulia na utazamie Mungu, Yesu na Roho Mtakatifu. Chukua wakati **ukiomba kwa Roho.** Tumia kipawa cha kunena kwa lugha mpya.
Soma Neno la Mungu ukimwomba Roho Mtakatifu kwa ufunuo. *(Efe. 1:17-18)* omba kulingana na Maandiko Matakatifu ambayo unasoma. Omba ufahamu yale ambayo Mungu anasema katika kifungu hicho na kinakufaa kwa njia gani leo.
Tarajia kuwa Mungu anakusikiliza wakati unaongea Naye. Halafu ngojea Naye akujibu. ***(1 Yoh. 5:14-15)*** **[tukiomba-Anasikia]** kuwa na kalamu na kitabu kunukuu yale anayosema.
Shukuru kwa yale unasikia.

NI NINI KINACHONIZUIA KUSIKIA KUTOKA KWA MUNGU?
Dhambi ya maksudi. ***(Isa.59:2)***
Kutokusamehe mmoja kwa mwingine. ***(Matt.6:15)***
Uhusiano usiokuwa mzuri kati ya Mume na Mke. ***(1Pet.3:7)***
Ubinafsi. ***(James 4:3)***
Kujihuzisha na miungu mingine; yoga, uchawi wote kama kusoma bao, nyota na kadhalika. ***(Kut.20:3-5)***

SALA YA BWANA

Luka aliandika kuhusu Sala ya Bwana. Wanafunzi walimwambia: "*Bwana, tufundishe kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake*." ***Luka 11:1***
Katika **Matt. 6:9,** Yesu akawaambia: *"Basi, ninyi salini hivi:"*
Katika historia ya kanisa, hii sala imekaririwa kwa uaminifu na imani kuu. Pia imetumiwa kama mfano wa maisha ya maombi katika kanisa.

Katika sala hii, Yesu alipeana ufupisho wa mambo bayana yaliyo muhimu katika sala.

A. TUNA MTAZAMIA MUNGU na KUINGIA KATIKA UHUSIANO PAMOJA NAYE KWA NJIA YA YESU KRISTO, MWANA WAKE.
B. TUNAMWABUDU MUNGU.
C. TUNAOMBA UFALME WAKE UJE.
D. TUNATAFUTA MAPENZI YAKE
E. TUNAMSIHI MUNGU KWA AJILI YA MAHITAJI YETU
F. TUNAUTAFUTA MSAMAHA.
G. TUNAOMBA MSAMAHA.
H. TUNAOMBA UKUOMBOZI KUTOKANA NA ADUI.
I. TUNAMALIZA KWA KUABUDU.

Katika somo hili, tutaangalia na kutafsiri kila aya kulingana na Maandiko Matakatifu, na kuomba katika nuru ya ufahamu.

A. TUNAMTAZAMIA MUNGU na KUINGIA KATIKA UHUSIANO PAMOJA NAYE KWA NJIA YA YESU KRISTO, MWANA WAKE.

"Baba Yetu"

Yesu anatuleta katika ***uhusiano wa kijamii*** pamoja na Mungu Mwenyezi, Muumba wa Vyote, kwa njia Yake Yesu Mwenyewe. Tunatakikana kumuita Mungu, "Baba Yetu". Tunapokea "*Roho kwa kufanywa wana, ambaye kwa huyo twalia, Aba, yaani, Baba*". ***(Rum. 8:15).*** Tunapewa hakikisho la mahali katika Jamii ya Mungu. Tunapowaza juu ya uhusiano huu, tunajawa na hali ya kumuogopa Mungu tunapotambua urithi ambao amatupatia. *"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu;"* ***(1 Yohana 3:1.)***

"Uliye mbinguni".

Mungu anakaa mbinguni, ***nyumbani Kwake Milele***. *"Mbinguni ni kiti changu cha enzi na duniani ni mahali pa miguu Yangu."* ***(Is.66:1-2).*** Tunamwona Mungu katika utukufu Wake wote Akiwa ameketi enzini, mbinguni, bali anatamani katika heshima hiyo yote kukaa na wanyenyekevu na waliofunjika moyo. Tunakumbuka kuwa Yesu tayari amefufuka na ameketi mkono wa kuume wa Baba katika ulimwengu wa Roho, **(*Efe. 1:20*)** na tumefufuliwa pamoja Naye na *"kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu"* **(*Efe.2:6*).** *"Wenyeji wetu uko mbinguni"* ***(Fil.3:20)*** na tunatakikana *kutafuta yaliyo juu Kristo aliko ameketi mkono wa kuume wa Mungu* ***(Kol.3:1-3).*** Tunayainua macho yetu kutoka kwa vitu vya duniani na kumtazamia Mungu.

Tunaanza kutafakari juu ya Maandiko yanayozungumzia vile mbinguni kulivyo.

Sio Ezekieli wala Yohana (wote waliopokea maono ya mbinguni) anaweza kupata maneno ya kufaa ya kuelezea uzuri wa yale walioyaona katika maono yao. Wanazungumzia vitu "kama" au "kama kuonekana". ***(Ez.1:27-28)***
Hata hivyo, tunapewa picha ya mahali penye uzuri usiosemeka na tunaweza kutafakari

juu ya yale wanayoelezea:

Wakaaji wake wanasujudu bila kukoma ***(Ufu.5:14)***
Utukufu wa Mungu na Mwana ndio nuru yake ***(Ufu.21:23)***
Katikati yake ni kiti cha Enzi ***(Ufu.4:2)***
Mto wa maji ya uzima unatoka kwenye kiti cha enzi na maji yake ni ya uponyaji ***(Ufu. 22:1-2)***

Huku ndiko nyumbani.

.

B. TUNAMWABUDU MUNGU KWA KULITUKUZA JINA LAKE

"Jina Lako litukuzwe."

Jina Lake ni Kuu. Yesu anatwambia tusifu na tuabudu kwa kuheshimu Jina la Mungu. [kutukuza: kufanya liwe takatifu, kutakasa; Gk.#37 SC]

Tunazo picha zilizo wazi kuhusu ibada ya huko mbinguni ambako viumbe wenye uhai wanaliheshimu Jina la Bwana. ***Ufu.4:8:*** *"Hawapumziki mchana na usiku, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuweko na aliyeko na atakayekuja!"*

JINA LA MUNGU

Mungu alimwambia Musa jina lake ni **"MIMI NIKO AMBAYE NIKO."** ***Kut.3:14***
Kutoka wakati huo Mungu amejifunua katika Jina lake katika njia mbali mbali na katika namna nyingi. Jina Lake linadhihirisha Asili Yake na tabia Yake.
Majina mengine ya Mungu:

Yehova - Yireh: BWANA atapeana ***Mwa.22:14*** *I AM IS OUR PROVIDER.*
Yehova - Rapha: BWANA akuponyaye ***Kut.15:26***
Yehova - Nissi: BWANA ni ushindi wako ***Kut.17:15***
Yehova M'Kaddesh: Mimi ni BWANA akutakasaye ***Lawi.20:8***
Yehova - Shalom: BWANA ni amani yetu ***Waamuzi 6:24***
Yehova - Tsidkenu: BWANA ni haki yetu ***Yer.23:6***
Yehova - Rohi: BWANA ni Mchungaji wangu ***Zab.23:1***
Yehova - Shamma: BWANA ambaye yupo ***Ezek.48:35***

[Tafadhali jua kwamba YEHOVA sio jina la tafsiri ya hakika ya Jina la BWANA kutoka kwa kiebrania Agano la Kale. Mfano huu wa jina ndio unaojulikana. Katika siku za hivi karibuni, YAHWEH limetimika kama tafsiri ya hili Jina. Hili limetolewa kwa konsonanti 4, YHWH, ambapo ndivyo jina hilo linavyoonekana katika maandishi ya Asili.
Waaminio wa kiyahudi wa nyakati za Agano la Kale hawakutumia Jina hilo kumaanisha BWANA walitumia Jina ADONAI, ambalo linamaanisha Bwana. Katika tafsiri nyingi za Biblia, Jina la BWANA linaonekana katika herufi kubwa. Wakati ADONAI linapotafsiriwa katika lugha ya kawaida, linaandikwa Bwana, yaani herufi ya kwanza kubwa kisha zile zingine ndogo.]

JINA LA YESU

"Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani." ***(Is.9:6).***
"bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye ataitwa jina lake Imanueli" ***(Is.7:14).*** Mungu yupo pamoja nasi.
Bwana (mkuu katika mamlaka, kiongozi, bwana) **Yesu** (Yehovah ni wokovu) **Kristo** (Masihi, aliyeahidiwa) ni cheo kikamilifu alichopewa Mwana wa Mungu. Jina lake linapotambulika katika kweli, Baba anatukuzwa.

"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lipitalo kila jina; ili kwa

*jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba."(**Fil.2:11).***

Ndani ya Yesu, Mungu ametimiza yote ambayo alikuwa amejifunua katika Agano la Kale. Katika kweli, Bwana Yesu Kristo amefanyika Mpaji wangu, Mponyaji wangu, Ushindi wangu, Haki yangu, Amani yangu, Utakaso wangu, Mchungaji wangu, kila kitu kwangu. Yesu ametufunulia Jina la Baba. ***(Yohana 17:26)*** Aliomba kuwa Baba atuhifadhi katika Jina Lake. ***(Yoh. 17:11)*** Kuna usalama na ukombozi katika Jina Lake.
"Jina la BWANA ni ngome Imara; wenye haki hukimbilia wakawa salama." ***(Mith.18:10)***
"Yeyote atakaye liitia Jina la BWANA ataokoka." ***Matendo2:21***
Tunapoliinua Jina lake juu, Yesu atawavuta watu wote kwake. ***(Yoh. 12:32)*** Tunapomsifu Mungu na kuheshimu Jina Lake tunawapatia wengine nafasi ya kusikia habari Zake na hivyo hupata nafasi ya kumugeukia.

C.TUNAOMBA UFALME WAKE UJE

"Ufalme wako na uje".

Tunauombea ***ufalme ambao utaonyesha utawala wa Mfalme*** wa wafalme na Bwana wa mabwana. (**Ufu. 19:16**) Huyu Mfalme ndiye aliye na haki na mamlaka ya kuabudiwa. Yohana mbatizaji aliwaandaa watu kwa ajili ya kuja kwake masihi akiwaonya kuwa "*ufalme wa Mungu umekaribia". **(Matt.3:2).*** Yesu alianza huduma Yake kwa kuhubiri toba*"maana ufalme wa Mbinguni umewadia" **(Matt.4:17).*** Kwa maneno mengine, ufalme ulikuja (ulifunuliwa) katika Yesu, Mfalme.

Kwa Matendo na **Maneno** Yesu aliuonyesha Ufalme wa Mungu.
Maneno Yake:
Alipeana mifano yakutupatia ufahamu wa Ufalme. ***Matt.13***
Alifundisha kuwa tunaingia katika Ufalme kwa njia ya Toba. ***Matt.4:17***
Alisema kuwa Ufalme wa Mungu umo ndani yetu, ***Luka 17:21*** na kwamba tunatakikana kuzaliwa mara ya pili ili tuweze kuingia katika huo ufalme. ***Yoh. 3:3,5***
Tuutafute Ufalme wa Mungu kwanza. Hili linatakikana kuwa lengo letu la kwanza katika maisha yetu. ***Matt.6:33***
Alifundisha kwamba kutii mapenzi ya Mungu ni muhimu na kigezo kikuu katika kuingia katika Ufalme wa mbinguni. ***Matt.7:21***

Matendo Yake:

Yesu alionyesha kwa matendo Ufalme wa Mungu kwa ishara za ukombozi kutokana na pepo wachafu (Matt.12:28) na kwa maponyaji.
1 Kor.4:20; *"Kwa maana Ufalme wa Mungu sio kwa Maneno tu bali katika Nguvu"*
Rum.14:17: Ufalme ni *"katika Roho Mtakatifu"* na uwezo wake unadhihirika kwa njia ya vipawa vya Roho. Ni lazima tuonyeshe matunda ya Ufalme. ***Matt.21:43***
Kufa kwake Yesu Kristo, kufufuka na kupaa kumetuinua juu kuwa vyombo vya Ufalme. Tunatakikana kuhubiri Injili ya Ufalme kwa *"mataifa yote"* ***(Matt.28:19)***; kwa *"kila kiumbe"* kwa ishara ***(Mk.16:15)***; na *"ndipo mwisho utakuja"* ***(Matt.24:14)***. Ufalme wa Mungu unachukua mahali pa ufalme wa nguvu za giza. ***(2 Kor.10:3-6; Fil.2:9-11)***

Yesu ataheshimiwa na watu wote na nguvu zote. ***Ufu.11:15***
Mwisho utawadia lini? ***1 Kor 15:24***

Ni nani atakayerithi Ufalme? ***Matt.25:34***

Huu ndio ufalme ambao tunaombea uje: Ufalme wa Mungu ambao ni *"haki, na amani na furaha katika Roho Mtakatifu"* ***(Rum.14:17).***

D. TUNAOMBA MAPENZI YAKE KUFANYIKA

"Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni."

Tunafahamu mapenzi ya Mungu kupitia kwa Neno Lake - Biblia. Tayari tumeona kuwa mapenzi ya Mungu makuu kwa ajili ya Ufalme na kwa watakatifu. Neno la Mungu linatubadilisha kwa kufanya upya nia zetu ili "***mpate kujua mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza, na ukamilifu" (Rum.12:2).*** Tunatakikana *"kuelewa yalivyo mapenzi ya Bwana"* ***(Efe.5:17).*** Tunapoupokea ufunuo kwa njia ya Neno la Mungu, tunafanyika zaidi kama Yesu na mapenzi ya Mungu yanafanyika hapa duniani.***2 Pet.1:3-4***: *"Kwa kuwa uweza wake wa uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu...."*

Neno la Mungu linafunua mapenzi yake Kwa:

Wale walio kwenye mamlaka ***1 Tim.2:1-6***
Wote waokoke ***1 Tim.2:4;2Pet.3:9***
Wafuasi wake *"basi, enendeni, ulimwenguni kote mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi"* ***(Matt,28:19-20).***

Yesu Anatii Mapenzi Ya Baba

Yesu aliweka wazi kuwa yote aliyosema na kutenda yalikuwa kulingana na mapenzi ya Baba. ***Yoh. 5:19; 14:10b***
Yesu anasema nini kujihusu? ***Yohana 6:38-40***
Katika sala tunatafuta kupambanua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya watu fulani na kwa hali fulani. Ni Neno lidumulo ndilo hufichua mapenzi ya Mungu (***Yoh. 15:7)*** na Yesu ameahidi Roho Wake atatufunulia yaliyo Yake. ***(Yohana 16:15)***

F. TUNAMSIHI MUNGU KWA AJILI YA MAHITAJI YETU

"Utupe leo mkate wetu wa kila siku".

Mkate wetu wa kila siku ni nini? Yesu anatwambia tusisumbukie mahitaji ya muda mfupi. ***Matt.6:25-32*** Ameahidi kuwa tukiutafuta Ufalme wa Mungu kwanza, basi mambo mengine tutaongezewa.***a.33***

Mkate wa uzima wa kweli ni Mtu.
Yoh 6:33: *"Kwa maana mkate wa Mungu ni Yule ashukaye kutoka mbinguni na kutoa uhai wake kwa ajili ya ulimwengu."* Yesu ni mkate wa uzima. Tunatakikana kula mwili wake na kunywa damu yake kila siku. ***Yoh. 6:50-56***
Yesu akasema: *"Maneno niwaambiayo ni Roho tena ni uzima" (****Yoh 6:63).***

Mkate unatumiwa mara nyingi kama mfano wa chakula cha roho katika Maandiko:
manna, meza ya mkate wa Wonyesho, mkate wa Pasaka (sasa ni mkate wa Meza).
Ayubu*"Aliyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya chakula chake" (****Ayubu 23:12).***

Mungu anatualika tule kulingana na unono alionao. *"Kwa nini kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula?Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha?Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono"* ***(Is.55:2).***

Katika sala omba Mungu kila siku kwa ajili ya chakula chako cha Roho. Chakula chake kitunze roho na nafsi zetu.
Neno lake pia ni mbegu yetu ya kupanda katika maisha ya watu wengine. Ni *"mbegu kwa mtu apandaye na mkate kwake alaye chakula" (**Is. 55:10).***

E. TUNATAFUTA MSAMAHA

"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wadeni wetu".

Tunatambua kuwa ***kuwasamehe wengine ni jambo la msingi*** kwetu kupokea msamaha wetu. Yesu anasisitiza hili katika ***Matt.6:14-15, Mk.11:25-26*** na katika mfano wa msamaha. ***Matt.18:21-35*** Mara nyingi uponyaji na ukombozi huja kwa mtu ambaye amewadhuru, ama mtu ambaye wanamudai kitu. Kuna wakati ambapo madhara ama kutumiwa vibaya ni kwa njia kubwa sana ambapo tunahitaji neema maalum kutoka kwa Bwana ili tuweze kusamehe. Tunapochagua kusamehe, Mungu hupeana neema hiyo, kutuwezesha kutoa msamaha wa kweli. Msamaha haumaanishi kukubaliana na kosa lililofanywa. Mungu anachukia dhambi, lakini anamsamehe mtenda dhambi.

Tunapoutazamia msalaba, tunaona kwamba Yesu alifilia dhambi za ulimwengu mzima.
Hii ni pamoja na maovu unayofanyiwa.

*"Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alitufilia" (**Rum. 5:8).***
Kwa njia ya neema ya Mungu, tunapomsamehe mtu, uchungu na udhuru unaondoka katika mawazo yetu.

H. TUNAOMBA KUONGOZWA

"Usitutie majaribuni".

Mungu hawezi kutujaribu!

*"Maana kila kilichomo duniani – tama ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima – havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia" **(1 Yoh. 2:16).***
*"bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele" **(a.17).***
Tunajaribiwaje? ***Yakobo 1:14***
Ni ushauri gani ambao Paulo anamtolea Timotheo? ***2 Tim.2:22***

*"Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi natukaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." **(Ebr.4:15-16).***

Twajua:
Tumesamehewa dhambi
Sisi ni wana na binti za Mungu
Tumeketishwa pamoja ka Kristo katika ulimwengu wa Roho
Yesu yuko mbinguni akituombea
Damu yake iko juu ya kiti cha rehema

Yesu ameshinda nguvu zote za yule mwovu.

G. TUNAOMBA KUOKOLEWA NA YULE MWOVU

"Utuokoe na yule mwovu".

Yesu aliombea ulinzi wetu: *"Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu" **(Yoh. 17:15).***
Neno la Mungu linakaa ndani yetu na tunashinda kwa damu ya Mwana Kondoo (tukijua kile Yesu ametufanyia Kalvari) na neno la ushuhuda wetu (kuwaambia wengine kuhusu yale ambayo ametufanyia, ama kukiri neno la rhema kama ilivyo katika ***Matt.4:4,7,10***

wakati Yesu alivyojaribiwa nyikani.)

Wakati tunapojaribiwa, omba mlango wa kuepuka, *1 Kor.10:13*
Rum.8:33-34 *"Ni nani atakaye washutumu wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye wakuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea."*

Tunapoona kile ambacho Yesu ametufanyia tunamtazamia yeye, tukitambua nguvu zake kuu za kutukomboa na kutuokoa na yule mwovu.
Tunafanya nini? ***Yakobo 4:7-8***

Tunatumia silaha ambazo Mungu ametupatia, maana "*ni kuu katika Mungu katika kuangusha chini ngome"* ***(2 Kor. 10:4).***
Tunatia *"kila wazo kuwa mateka hadi litii Kristo" (**a.5).***
Tunatumia *"upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu."* ***(Efe.6:17).***
Tunakataa kila uongo wa yule mwovu. Mungu anatuokoa na yule mwovu tunapomtumainia.

Ujasiri wetu ni gani katika Kristo Yesu? ***1Yoh.5:18-20***

Ni nani anayeushinda ulimwengu? ***1 Yoh.5:5***

Tambua ukweli huu na *"ushinde uovu kwa wema"(Rum.12:21).*

I. TUNAMALIZA KWA KUSUJUDU

"Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina."

Tunasifu na kumuinua Mungu, tukimpa utukufu wote

Tumeingia katika ufahamu wa Ufalme Wake, kuujua uweza Wake na kuinua utukufu Wake

Tumeingia katika uhusiano wa kijamii ya Mungu Mwenyezi na tumemsujudia Baba yetu wa Mbinguni
Tumeomba ufalme wake uje hapa duniani
Tunakua katika maarifa ya mapenzi yake, tukimtumikia Mungu Mkuu na kuwa chombo chake ambacho mapensi Yake yanatimizwa kwa njia ya maombi duniani
Tunashiriki katika "nafaka iliyo safi", chakula chetu
Tunatubu dhambi zote na kupokea msamaha wa Mungu kwa kigezo kuwa tunasamehe wengine
Tunakabiliana na udhaifu wetu, kukwepa mitego ya majaribu Bwana anavyotuongoza, akituonya kupitia kwa Neno Lake
Tunaingia katika vita vinavyostahili

Tunamaliza maombi tukiwa tumenaswa katika kumsujudia Mungu wetu Mkuu na Mfalme.

ZOEZI LA BINAFSI

Enda mahali palipotulia pekee yako. Andika Sala ya Bwana huku ukiacha nafasi baada ya kila mstari. Katika nafasi hizo andika mawazo, sehemu za kuombea, Maandiko Matakatifu na cho chote kinachokuja katika fahamu zako. Nena na Mungu unapofanya zoezi hili. Kumbuka, maombi ni mawasiliano na Mungu. Omba Mungu akuzungumzie na akuongoze.

KUOMBA KULINGANA NA MAANDIKO.

NENO LINALODUMU
Yesu alisema katika ***Yoh.15:7****, "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa".* Yesu anatoa tiketi iliyo wazi ya njia ya maombi kujibiwa. Hata hivyo, hiyo tiketi iliyo wazi iko juu ya msingi wetu wa kukaa ndani ya Kristo na maneno Yake (rhema) kukaa ndani yetu.

Matokeo ya maombi ya namna hii humtukuza Baba,
Tunazaa sana, yanadhihirisha kuwa wanafunzi hakika *(a.8)*.

LOGOS na RHEMA
Katika Agano Jipya, majina mawili ya Kiyunani yanajitokeza ambayo yametafsiriwa na jina neno. Majina ya Kiyunani ambayo yametumiwa ni **logos** na **rhema**.
Yoh. 1:1*: "Hapo mwanzo kulikuweko Neno **(logos)**...".* Hapa logos inazungumzia Yesu. Katika aya zingine nyingi, neno logos linatumika na linatafsiriwa "neno",(karibu mara 200). Pia hilo jina la logos limetafsiriwa katika majina mengine kama:- mawasiliano, mafundisho, swali na kama majina mengine kumi na nane. Logos linazungumzia Biblia kuwa "Neno la Mungu", Neno la Mungu ambalo limefunuliwa, lililoandikwa kwa ajili yetu.

Katika ***Matt.4:4***, Yesu anasema, "*Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno **(rhema)** litokalo katika kinywa cha Mungu".* Hapa Bwana anatoa ufafanusi wa jina rhema, neno linatoka katika kinywa cha Mungu, neno la sasa, neno lililohuishwa.

Hilo jina Rhema limetumiwa karibu mara sitini.
Kwa mfano:
Rum.10:17**: "Imani huja kwa kusikia na kusikia kwa neno (rhema) kuhusu Kristo, (ama rhema ya God)".**
Mariamu alimjibu malaika katika ***Luka 1:38:*** *"Na iwe kwangu vile ulivyosema".*
Rum.10:8: *"Neno li kribu nawe, kinywani mwako na moyoni mwako...".*
Ni ufunguo gani Yesu alitupatia katika kuomba kulingana na Maandiko Matakatifu? ***Yoh.15:7***

KUOMBA KULINGANA NA MAANDIKO MATAKATIFU
Kuomba kulingana na Maandiko ni njia moja ya kuwa mtu wa nidhamu katika kusoma na pia njia ya kupata ufunuo wa maarifa ya mapenzi ya Mungu. Kwa pamoja safari na njia huleta kutimia na hali ya maombi kujibiwa.

VILE INAVYOFANYIKA:

Hivi majusi, nilikuwa nikiendesha gari kuenda katika maombi ya asubuhi. Nilikuwa kwa haraka nina vaa silaha zote za Mungu. ***(Efe.6:13)***. Nilipochukua ngao ya imani, nikaanza kukiri imani katika Yesu Kristo juu ya jamii yangu na kuanza kumwambia Mungu juu ya kila mmoja katika jamii yangu. Ghafla, nikakumbuka maneno ya Mungu kwake Abramu katika ***Mwa.15:1****"Mimi ni ngao yako".* Hili lilinifurahisha sana nilipotambua kuwa Mungu mwenyewe ni ngao yetu, na kwa kuvaa ngao ya imani hakika ilikuwa ni kumukubali Mungu kama ngao yangu. Kuwa karibu na Mungu kama ngao ni jambo la kufurahisha. Cha ziada, nikakumbuka kwamba Mungu alimwita Abramu kama baba wa jamii ***(Mwan.18:19)***, na ikaonekana Mungu alikuwa akiniambia, Mimi ni ngao ya jamii yako pia. Bwana asifiwe! Kwa uhuru mkuu na furaha, nilimshukuru kwa ajili ya kuwa ngao ya jamii yangu. Niliposhiriki ufahamu huu uliohuishwa kwa na kikundi cha

maombi, walibarikiwa na kutiwa moyo.

IMANI NDIO UFUNGUO:
Yesu anafundisha juu ya maombi katika ***Marko 11:22-25***.
(i) Ufunguo ni imani ndani ya Mungu. *"Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana".**(Ebr.11:1)*** Kwa maneno mengine, **imani ni kuamini Mungu katika msingi wa lile Neno Lake linavyotwambia kumuhusu na kumfunua alivyo.**

(ii) Pili, *"Imani huja kwa kusikia, na kwa kusikia Neno la Mungu" **(Rum.10:17)***. Lakini hili ni Neno la Rhema kutoka kwa Mungu, Neno lililohuishwa ambalo huleta imani tunaposikia sauti Yake.

(iii) Twaomba, tukiamini kuwa tumepokea kile ambacho tumeomba; na yatakuwa yetu.***(Mk.11:24)*** Tunaomba kulingana na vile tumepokea Neno la Mungu mioyoni mwetu. Tunajua tunaomba kulingana na mapenzi ya Mungu na tunaujasiri kwamba anatusikia na atajibu. Hatuombi kwa imani isiyoona maana imani ya biblia ina msingi wake katika Neno la Mungu.

Maombi ya bidii ni maombi yanayofanywa kwa imani, na imani inatokana na kukua kulingana na ufahamu wa Neno linavyofunuliwa kwetu ama kuhuishwa na Bwana katika ufahamu wetu. Katika njia hiyo tutakuwa tunaomba kulingana na Maandiko Matakatifu.

Wakati ambapo tunaomba Sala ya Bwana tunakuwa tunaomba kulingana na Maandiko. Wakati mwingine inatosha kuomba ukitumia maneno hayo jinsi yalivyo, yaani kwa kuelewa kila mstari ulivyoandikwa na msingi wake na kuomba kulingana na ufahamu huo.

TUNAOMBA NINI?
Kuna sehemu nyingi sana za kuanzia katika Maandiko. Tutaanzia katika ***Rum.12:1-3.***
1. ***Itoeni miili yenu***:

Maandiko yanatwambia tutoe miili yetu kama dhabihu iliyo hai na takatifu, ya kumpendeza Mungu. Hii ni ibada yetu. Sipati maneno ya kutosha kuomba ila maneno katika Maandiko: "Bwana, ninajitolea mwenyewe kwako, mwili wangu wote kama dhabihu iliyo hai kwa njia ya rehema zako. Ninakushukuru, Bwana, kwamba mimi ni mtakatifu na ninakubalika Nawe. Bwana ninakuabudu".

2. ***Mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu:***

Aya ya 2 inatwambia tugeuzwe kwa kufanywa upya nia zetu. Hii ni kinyume kabisa na mawazo na njia za dunia. Ninatambua kuwa Roho Mtakatifu ananipa roho wa kufanywa upya nia yangu ***(Efe.4:23)***, na ninamshukuru kuwa huyu ni roho wa upendo, nguvu na nia njema ***(2Tim.1:7)***. Nia yangu inapofanywa upya kwa njia ya kutafakari juu ya Neno la Mungu, ninawezeshwa kujua ni nini mapenzi ya Mungu.
Nitajuaje mapenzi ya Mungu? Kwa njia ya kuendelea kukua katika kulijua Neno. Hili halimaanishi kuwa lazima nijue Maandiko yote. Ninaweza kusoma na Mungu ametuandikia Neno Lake kwetu sisi. Nikihitaji msaada zaidi wa kupata majibu katika maandiko kuna mistari katika Biblia na kamusi za kunisaidia.

3. ***Ninaomba katika makubaliano na Mungu:***

Soma ***Matt.6:25-34***. Nikiwa nimesumbuka kwa ajili ya mambo ya kitambo kidogo,

ninaomba kulingana na aya ya 31 na kushukuru Mungu kwamba anajua mahitaji yangu. Na katika utiifu wa imani, ninautafuta ufalme wa Mungu kwanza na haki Yake, kisha nijiandae kwa hizo changamoto za siku hiyo. Hizi aya za Maandiko zinatakikana kutumiwa kila wakati katika maombi maana ni rahisi wakristo kujiingiza katika kujisumbua na mambo ya dunia hii.

Fil.4:6-7 inatupatia misingi zaidi ya kutokujisumbua na tujue jinsi ya kuomba kulingana na maandiko. Tunatakikana kutoa haja zetu kwa shukrani. Tunajua Mungu tayari ametusikia tunapopata "amani rohoni mwetu".

4. ***Ufanye huo mstari kuwa wako:***

Soma ***Efeso Sura ya 1***, na kwa njia ya maombi soma kutoka mstari wa kwanza. Paulo ananiandikia mimi, mtakatifu hapa Nairobi, ambaye ni mwaminifu katika Kristo Yesu. Ninapoendelea na kuweka jina langu katika kifungu hicho; ninahimizika na kuhuishwa na Neno la Mungu. Mara nyingi humalizia katika sifa na kuabudu kwa sababu nataka kumbariki Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo ambaye amenibariki na kila Baraka ya rohoni katika ulimwengu wa roho ***(a.3)***.

5. ***Mpate kujua mapenzi ya Mungu yalivyo***:

Kol. 3 ni kifungu cha ajabu kuomba, kwa utiifu tukifanya yale maandiko yanasema:

(i) Ninatambua kuwa nimefufuliwa na Kristo na ninatakikana kutafuta yaliyo ya juu;

(ii) Ninaingia katika ulimwengu wa roho, nikitambua kwamba nimezaliwa kwa Roho na Mungu Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu: maisha yangu yamefichwa ndani ya Kristo. Ninaingia katika chumba cha ndani ndani yake na kuwasiliana na Mungu.

(iii) ***a.5-9***, Ninakiri dhambi zangu kwa Mungu, nikichukia uwepo wake katika maisha yangu, nikiachana kila uasi, na kuzima nia zote mbaya na hisia mbaya.

(iv) Ninajitambulisha na Mtu mpya ambaye amefanywa upya katika Kristo Yesu ***(Efe.2:10)***, nikivaa utu wa kimungu ambao umeandikwa katika mistari ***a.12-15***.

(v) ***a.16*** inanieleze *"na Neno la Kristo likae ndani yenu kwa wingi"*; hili ni logos hapa. Katika maneno mengine, ninajizamisha katika kusoma Maandiko; ninayasoma kwa njia ya Maombi, nikimuomba Mungu ajifunue Mwenyewe kwa njia ya Neno Lake. Pia Maandiko yanatuhimiza kuimba nyimbo na saburi ambazo zinadhihirisha Neno.

(vi) ***a.17*** unaniingiza katika matendo.

Kuomba kulingana na Maandiko ni njia ya nguvu; inafurahisha; ni ya ufunuo; inaelekeza; inatujulisha mapenzi ya Mungu ni nini: ambayo ni mema, ya kupendeza, na makamilifu *(Rum.12:2)*.

6. ***Kila mmoja amepokea kiasi cha imani:***

Tambua katika ***Rum.12:3***, kila mmoja wetu amepokea kiwango cha imani. Jina la Kiyunani kumaanisha imani ni *pistis* bali linatoka kwa neno *peitho*, kusihi, kuwa na ujasiri. Mtume anasema kuwa kila mmoja amegawiwa kiasi cha imani kutoka kwa Mungu. Hicho kiasi kinatosha kumtumikia kwa njia ya vipawa vilivyomo katika ***Rum.12***. Mungu ashukuriwe kwa ajili ya imani ambayo ameweka moyoni mwangu.

Ufahamu wetu wa Mungu utakuwa katika misingi ya ufunuo wa Maandiko. Ujasiri wetu ni katika Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Mungu wa Biblia.

KUVAA SILAHA ZA MUNGU

Wengi wetu tumeelekezwa kuvaa silaha za Mungu wakati wa maombi kila siku

(Efe*.6:10-18)*. Utafanya haya aje? Je utakariri kila silaha, ukimwambia Mungu juu ya kuvaa Chepeo, dirii, viatu n.k. ama kwa njia ya Maombi na kwa kutafakari unatumia ukweli huu wa maandiko katika maisha yako na kuleta mawazo yako na mipango katika makubaliano na mapenzi ya Mungu kwako siku hiyo. Kwa mfano, chepeo hakika hufunika kichwa, ambayo huwakilisha kituo cha mawazo na nia. Cha ziada, ni chepeo cha wokovu ambacho huleta ufahamu mkubwa wa ukweli wa Biblia wa kutambua na kuwazia juu yake.

Isaya 26:3 anatwambia kuhusu tunda la nia yetu ambayo unamtazamia Mungu. ***Kol.3:1-2*** inatwambia tufikirie juu ya mambo yanayotoka juu. Kwa kuchukua tu mfano wa kofia na kifanya kitendo, kwa ishara ya chepeo la wokovu haiwezi kutenda cho chote. Bali kukiri na kuamini Neno la Mungu kuhusu wokovu, kuhusu kufanywa upya nia, na kutafakari juu ya Neno lake usiku na mchana, itafanya kazi kuu, likitujenga kujikinga na yule mwovu, na mawazo mabaya.

BALI MJAZWE NA ROHO

Efe.5:18 inatwambia tujazwe na Roho yaani tukisemezana katika saburi, tenzi za rohoni huku tukimwimbia na kumshangilia Bwana miyoni mwetu. Je! Umetambua kuwa pambio nyingi hunukuu maandiko matakatifu? Nyingi ya saburi na tenzi za rohoni huonyesha ukweli mwingi wa Biblia na mafundisho?

Sifa na shukrani na nyimbo za kuabudu nyingi yazo ni maombi. Tunapofanya yale Maandiko yanasema – tunaimba maandiko – tunajazwa na Roho.

MAOMBI MENGINE KATIKA MAANDIKO

1. Kanisa La Kwanza Liliomba Kulingana Na Maandiko:

Katika ***Matendo 4***, kikundi cha waaminio kilinukuu sehemu za Maandiko katika maombi yao. Katika **aya ya *24***, walinukuu ***Kutoka 20:11*** na ***Zab. 146:6***, halafu katika aya ya ***25-26***, ***Zab. 2:1-2*** imenukuliwa.

2. Paulo anatuombea:

Maombi ya Paulo kwa ajili ya kanisa ni ya kutia nguvu. Mara nyingi mimi huomba maombi yayo hayo kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili ya kanisa.

Efe.1:15-19: Paulo anahuzisha shukrani katika sala, kukiriri na maombezi katika sala yake. Anatuombea kwamba macho ya mioyo yetu yatiwe nuru, tujue tumaini la mwito Wake lilivyo kwa ajili ya watu Wake.

Efe.3:14-21 Paulo katika sala zake anamtukuza Mungu; akifahamu nguvu za Mungu na kusudi Lake. Ni kwa sababu ya utajiri wa utukufu wa Mungu unaomfanya Paulo aamini kwamba atajibu maombi. Jawabu litakuja katika nguvu na litakuwa ni la Roho.

Hili ombi linatuweka ndani kabisa katika pendo la Kristo. Uzima wa Mungu utatiririka ndani ya maisha ya watu Wake. Mungu hatashiriki utukufu wake na mtu ye yote lakini anawamiminia bure wale waliomo ndani ya Kristo. Wakristo hawamo tena “kulingana na mwili bali kulingana na Roho”. Tambua kwamba nguvu zile ambazo Mungu hutumia kujibu maombi yetu tayari inafanya kazi katika waaminio. Si ajabu Paulo anasema “*atukuzwe katika kanisa”.*

Katika ***Efe.6:18***, Paulo anatuhimiza kuendelea katika sala kwa ajili ya watakatifu wote. Tazama katika ***Fil.1:3-11*** kwa mawazo ya kusaidia kuwaombea watu. Sio: "Bwana bariki mtu fulani na uwafanye wafurahi", bali omba "kwamba upendo wa watu ukaongezeke zaidi na zaidi katika kumjua na katika upambanuzi".

Tena katika Wakolosai, Paulo anaendelea katika sala ya ufahamu kwa ajili ya kanisa. Maombi ya shukrani, maombi ya kuongozwa katika ufahamu na ya ufunuo hutiririka pamoja.

Paulo hawezi kujizuia bali anaingia katia sifa kwa Mungu Mkuu anayefanya mambo haya yawezekane.

Efe.3:21 ***Fil.4:20*** ***Rum.11:36*** ***1Tim.1:17*** ***Rum.16:27***

Yuda pia hawezi kujizuia bali anaingia katika usemi mkuu wa sifa, kukiri, kusujudu na kuabudu ***(a.24-25)***.

"Atukuzwe, Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu." Amina ***(Efe.1:3).***

ZOEZI LA MTU BINAFSI:

Chagua sehemu ya Maandiko na uende mahali palipotulia peke yako na Mungu. Omba kulingana na Maandiko. Unaweza pia kupenda kuandika ombi kwa msingi ya kile ambacho Maandiko yanasema.

Aina ya maandiko ambayo unaweza kutumia:

Mwa.15:1-6; ***Mwa.32:24-32;*** ***Kutoka.33:13-23;***

Yosh.5:13-15; ***Zab.23:1-3;*** ***Zab.23:4-6;***

Zab.27:4-6; ***Isaya 6:1-8;*** ***Isaya. 43:18-19;***

Yer.29:11-14; ***Yer.31:31-34;*** ***Hos.6:1-3;***

Yoeli 2:28-32; ***Yoh. 10:9-11;*** ***Yoh.10:14-17;***

Rum.10:9-11; ***Efe.1:17-19;*** ***Efe.3:14-21;***

Fil.3:10-14

Haya ni Maandiko machache tu miongoni mwa mengi ambayo yanatia nguvu katika maombi, yakiwa na msingi wa kusikia kile ambacho Mungu anasema katika Maandiko Matakatifu.

SAUMU au MFUNGO

Jina "**saumu**" latokana na neno la Kiebrania "tsuwm" kumaanisha "kufunika kinywa" (Strong Concordance #6685); na kwa Kiyunani "nesteuo" kumaanisha "kujinyima chakula" (SC #3522)
Derek Prince anaelezea saumu kuwa "*kujitolea kujinyima chakula kwa ajili ya makusudi ya kiroho."*.

SIKU YA UPATANISHO / SAUMU
Siku ya Upatanisho iliwekwa kwa kalenda ya Wayahudi kama ***siku ya mfungo*** wakati watu walipotambua kwamba hawawezi kufanya lo lote kujikomboa kutoka kwa dhambi. Siku hiyo, Mungu alisema, *"Mtajitaabisha roho zenu"* ***(Lawi.16:29).*** Walihitajika kunyenyekea mbele za Mungu. ***(Lawi 23:26-29)*** Kuna sehemu nyingi katika Agano la Kale kuhusu **siku hiyo ya mfungo / Upatanisho**. Hii siku ilikuja ikawa tabia ya kila wakati kukutana na Mungu. Hii ni Saumu ambayo Paulo anazungumzia alipojaribu kumuonya yule nahodha wasiendelee na safari kwa sababu ya hali mbaya ya hewa. ***(Matendo 27:9)***

SAUMU KWA JUMLA KATIKA AGANO LA KALE
Kuna vivungu vingi vinavyonena juu ya saumu kando na siku ya kawaida. Katika kila hali, kuna jambo maalum la kutesa nafsi zetu mbele za Mungu: katika toba, kutafuta ufunuo na mwongozo, kumsihi Mungu kwa ajili ya mahitaji, katika kuomboleza. Mara nyingi mfungo ulihuzishwa na kuvalia magunia na majivu, kuonyesha kunyenyekea kwa mtu binafsi. Mfungo ulikuwa wakati wote unamaanisha kuleta mwili wa asili chini ya utiifu wa Roho wa Mungu ndani ya mtu; kuileta nia ya mwili katika kutii.
Ndipo Daudi akasema: *"Nilijitesa nafsi yangu kwa kufunga"* ***(Zab.35:13)*** *"na kuiadhibu roho yangu kwa kufunga"* ***(Zab.69:10).***

Kuna saumu aina tatu katika Maandiko Matakatifu:
(a) SAUMU YA KAWAIDA
(b) SAUMU MAKINIFU
(c) SAUMU HALISI

(a) SAUMU YA KAWAIDA:
Inahuzisha **kujinyima chakula**, lakini sio vinywaji. Mfano Yesu nyikani *"hakula cho chote"* ***(Luka 4:2)*** na baadaye *"Akasikia njaa".*

(b) SAUMU MAKINIFU:
Inahuzisha kuchunga kile mtu anakula kwa wakati fulani. Kwa mfano, Danieli katika kuomboleza *"hakula chakula kitamu, wala nyama wala divai" hata majuma matatu (****Danieli 10:3).***

(c) SAUMU HALISI: ni **kujinyima chakula pamoja na vinywaji** kwa muda fulani. Mfano ***Matendo 9:9*** inanukuu kwamba Sauli *"hakula wa kunywa"* kwa siku tatu.
Esta anatuma ujumbe "*msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana"* ***(Est. 4:16)***
Ezra "*hakula mkate, wala hakunya maji"* ***(Ezra 10:6)*** alipoomboleza kwa ajili ya dhambi za watu. [Siku tatu ndizo siku halisi za kukaa bila maji, bila kusaidiwa na Roho.]

Musa alikuwa katika Mlima wa Sinai *"na BWANA siku arobaini mchana na usiku; hakula mkate wala kunywa maji"* ***(Kut.34:28).*** Tunaweza tu kusema kuwa hii saumu

liliwezekana kwa msaada wa Mungu maana alikuwa katika uwepo wa BWANA (na BWANA).

SABABU ZA KUFUNGA

1. TUNAFUNGA ILI TUKUTANE NA MUNGU

Zek.7:5: *"Je! Mlinifungia mimi kwa lo lote – mlinifungia mimi?"*
Arthur Wallis anasema: *"kufunga kuna njia ya kutuachanisha na ulimwengu wa asili ili mawazo yetu yakaegemee, kukutana na Mungu na ulimwengu usioonekana ambao Yeye ndiye Mkuu."*

Saumu kulingana na mpango wa Mungu ni yake: ambapo **tunajitenga kwa ajili Yake, kumuhudumia, kumuheshimu na kumtukuza, kutimiza mapenzi Yake.**
Matt.6:18: *"Baba yenu aonaye sirini atawajibu kwa wazi"* kwa mfungo wa aina hii.

2. KWA UTAKASO WA KIBINAFSI.

Zab. 69:10: *"Nilipolia na kuiadhibu roho yangu kwa kufunga."*
Saumu ya aina hii huleta toba na kuomboleza.

3. KUUNGAMA DHAMBI ZA TAIFA.

Wana wa Israeli walifanya nini walipokuwa wakiungama dhambi zao wenyewe na dhambi za baba zao? *Neh.9:1-2*
Ezra alijinyenyekeza namna gani alipolilia taifa? ***Ezra 9:3-6***
Samueli alimwita nani kufunga alipoamua taifa kwa ajili ya dhambi zao? ***1 Sam. 7:5-6***
Danieli alimwelekezea Bwana Mungu uso wake *"ili kutaka kwa maombi, na dua, pamoja na kufunga, na kuvaa nguo za magunia na majivu"* akiomba huruma za Mungu kwa ajili ya wana wa Israeli ***(Dan.9:3-5).***

4. ILI MUNGU AKUSIKIE.

Saumu inaleta udharura katika kuomba kwetu na hupeana nguvu katika kuitana kwetu. Kufunga ili umtafute Mungu inaonyesha tumemaanisha katika kumtafuta Mungu. Bwana anasema, *"nigeukieeni kwa mioyo yenu yote, kwa kufunga, kwa kulia na kuomboleza"* ***Yoel 2:12. a.15*** *"Takaseni saumu"*
a.17 *"Na waseme, 'Uwaachilie watu wako, Ee BWANA'."*
Saumu aliyoichagua Mungu ***Isa.58:3b-5,*** Bwana anawakosoa watu Wake kwa sababu ya saumu yao yenye nia nyingine na mambo mengine. ***a*9** Anatuahidi kutujibu wakati tutakapofunga vile anavyotaka.

5. KUBADILISHA NIA YA MUNGU.

Wakati Yona alipowahubiri watu wa Ninawi, waliamini *"wakamsadiki Mungu, wakatangaza kufunga, wakajivika nguo za magunia."* ***Yona 3:5*** Mungu alifanya nini alipoona toba yao? **a*.10***
***1 Wafal 21:27-29*:** Kwa sababu Ahabu alitubu na kufunga, Mungu aligeuza adhabu yake na hakumuhukumu.
Kwa nini Daudi alifunga wakati mtoto alipokuwa anakufa? ***2 Sam.12:22***
Kufunga hakumushurutishi Mungu kutufanyia kitu.
Baadaya kuwasihi watu warejee kwa BWANA *"kwa kufunga na kulia na kuomboleza"*, Yoeli anasema: *"N'nani ajuaye kwamba hatarudi na kugeuka, na kutuachia baraka nyuma yake."* ***Yoeli 2:14.***

6. KUFUNGULIWA KUTOKA KWA UTUMWA.

Mungu anasema saumu aliyochagua itafanya nini? *Isa.58:6*
Yesu alisema wanafunzi walihitajika kufanya nini ili wamkomboe kijana mwenye roho chafu? ***Mk.9:29***

Esta aliwaambia wayahudi kufunga pamoja naye alipokuwa akijiandaa kwenda kwa mfalme kinyume na waraka uliokuwa umeandikwa kuwaangamiza. ***(Esta 4:16)*** saumu ilibadilisha historia na Mungu aliwafungua Wayahudi kutoka kwa mateso.

7. WAKATI WA VITA.
Mfalme Yehoshafatu alifanya nini? ***2 Nyakat.20:3***
Mungu alichukuliaje saumu yake? ***a.15, a.17***
Mfalme na watumishi wake waliitikia Mungu namna gani? ***a.18, a.21***
Nini ilimtendekea adui? ***a.22-23***
a.27-30 Na Mungu akatukuzwa.
Katika wakati wa vita, Ezra alimtafuta Bwana kwa ulinzi wa watu wanaposafiri kupitia katika maeneo ya adui. ***(Ezra 8:21-23)***

8. KWA MWONGOZO.
Wakati wa vita kati ya Israeli na kabila la Benyamini, wana wa Israeli "*walikuja katika nyumba ya Mungu na wakalia sana. Wakaketi hapo mbele za BWANA, wakafunga siku hiyo hata jioni..... ndipo wana wa Israeli wakauliza kwa BWANA..."* ***(Waam. 20:26-27).***

9. KWA UFUNUO.
Danieli alifunga ***(Danieli 10:1-3)*** na akakutana na mjumbe wa Mungu ***(a.10***) na kupewa ufahamu ***(v.14).***
Tambua kwamba ni wakati ambao Petro *"alitaka kula"* ***(Matendo 10:10)*** ndipo alipokea maono kutoka kwa Mungu ambao ulimwongoza kwenda kwa Mataifa kupokea Roho Mtakatifu.

10. KWA AFYA.
Danieli pamoja na wenzake hawakutaka kujitia unajisi kwa divai na vyakula vizuri vya meza ya mfalme. Mgao wa chakula chao uliwapa afya nzuri. ***(Danieli 1:8,15)***

Katika haya yote tunaona saumu ni zaidi ya kutii kanuni ambayo imewekwa na Mungu. **Inafanyika silaha kali na muhimu dhidi ya nguvu za giza na ambayo huleta ukombozi kutoka kwa utumwa wa kiroho na maseto.**

Kuombi na kufunga huleta msaada wa Mungu kwa niaba ya watu wa Mungu.

Tunamuona Mungu akitimiza ahadi Yake: *"Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina Langu watajinyenyekeza, na kuomba na kutafuta uso wangu, na kuziacha njia zao mbaya, ndipo nitasikia kutoka mbinguni, na kuwasamehe dhambi zao na kuiponya nchi."* ***2Nyakat.7:14.***

SAUMU ALIYOICHAGUA MUNGU
Katika ***Is.58:1-5***, Mungu anawaadhibu watu Wake maana saumu imafanyika jambo la kidini. Kusema kweli, watu walikuwa wakiwatusi wengine siku hiyo ya saumu wakati ambapo walihitajika kumuinua Mungu.
Mungu alitarajia watu Wake kufanya nini wanapokuwa wamefunga?
a6 a7 a9 a10
Mungu anaahidi nini kitakachotendeka tunapofunga njia anayotaka?
a8 a9 a10

YESU NA SAUMU
Wakati Yesu alipokuja hapa duniani, saumu ilikuwa imefanyika jambo la kidini na sherehe kwa wengi. Yohana Mbatizaji aliwapa changamoto Mafarisayo na Masedukayo

"kuzaa matunda yapasayo toba" ***(Matt.3:8).*** Yesu, pia, aliwakemea viongozi kwa kujionyesha wakati wanapofunga. ***(Matt.6:16)*** Alitoa maagizo mapya kuhusu matendo ya nje katika mfungo alipokuwa akiwarudisha watu kutambua kwamba **saumu ni kwa BWANA, kumtafuta BWANA, na kwa hivyo inastahili kuwa siku ya furaha na matarajio.**
Yesu alisema tutafanya nini? *Matt.6:17* **Matekeo ya mfungo wa aina hii ni nini?** *a.18*

YESU ANASISITIZA KWAMBA SAUMU NI KAMA KANUNI
Anasema: *"Mfungapo" (**Mt.6:16 & 17)*.
Alianza huduma yake na mfungo wa siku arobaini. Wakati huo ndio alishinda majaribu ya shetani na kujitokeza *"katika nguvu za Roho"* ***(Luka 4:14).*** Katika kujibu mashutumu ya mafarisayo na waandishi, Anasema: *"Je! Mwaweza kuwafanya wafunge walioalikwa arusini, akiwepo bwana arusi pamoja nao? Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi, ndipo watakapofunga siku zile."* ***(Luka 5:34-35).*** *Alileta sababu ya kufunga*- **kuutafuta uwepo wa Mungu** – kurudisha lengo.

SAUMU KATIKA MAISHA YA KANISA LA KWANZA
1. Sauli na Barnaba wanatumwa kwenda.
Roho Mtakatifu ananena wakati manabii na waalimu walipokuwa *"wakimhudumia Bwana na kufunga."* ***Matendo13:2*** Wanafunzi waliendelea kufunga na kuomba kisha, *"wakawawekea mikono juu yao"* na *"wakawatuma waende"* ***Matendo 13:3.***
2. Makanisa mapya yalipoanza kujipuka, Paulo na Barnaba waliwaweka wazee kila mahali *"kwa kuomba na kufunga."* ***Matendo 14:23.***
3. Katika ***2 Kor.11:27*** Paulo anasema kufunga ni sehemu ya maisha yake. Anazumgumza juu ya "Mfungo" (Siku ya Upatanisho) wakati alipokuwa mfungwa kwenye meli aliyoabiri. ***(Matendo 27:9)***

SAUMU LEO
1. ***Je! ni Roho Mtakatifu anayeniongoza***? Je! Haja ya kuomba imetokana na Mungu? ***Luka 4:1:*** *"Yesu aliongozwa na Roho kwenda nyikani."*

2. ***Je! Nia yangu ni kumtafuta Bwana***, kunyenyekea mbele za Mungu, ama kuwafanya wengine wanihurumie? ***Matt. 6:18:*** *"Baba yenu aonaye kwa sirini atawajibu kwa wazi."*

3. ***Ninataka kupata nini kiroho*** katika hii saumu? ***Fil.3:12:*** *"Bali nakaza Mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu."*

4. ***Je! Ninayalenga mahitaji yangu tu ama ya wengine pia***? ***Is.58:10:*** *"Kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani, na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri."*

5. ***Je, azma yangu kuu ni kumpendeza Bwana katika saumu hii***? ***Matendo 13:2:*** *"walipokuwa wakimhudumia Bwana na kufunga."*

CHA KUTARAJIA UFUNGAPO
Siku za kwanza chache utasikia ***njaa***. Kutakuwa na ***dalili za kuachwa*** kwa wale ambao wana uzoefu wa kutumia vyakula fulani au vinywaji kama kahawa na chai. Wakati mwingine ***utaumwa na kichwa*** mtu anapojinyima kwa siku chache. Mara nyingi kutakuwa na ***unyonge, kukosa nguvu***. Baada ya siku chache mwili unazoea na utaanza kutumia mafuta yaliyoko mwilini. Wakati mwingine ***mwili huuma.*** Wakati wa mfungo mwili hujiosha wenyewe kutokana na uchafu. Baada ya muda mwili husikia kuendelea

kufunga. ***Njaa itarudi wakati unapokaribia kufuturu*.**
Ni jambo la muhimu **kuongeza viwango vya vinywaji** wakati unapofunga. Maji husaidia katika kuosha na mchungwa yatasaidia upungufu wa vyakula katika mwili.

JINSI YA KUFUTURU
Kwa sababu mwili unakuwa umebadilika sana wakati wa mfungo, ni jambo la muhimu kufuturu kwa viwango au kwa mgao**. Njaa inapoamka katika mwili, ni muhimu kukabiliana na tamaa yako hadi mwili uweze kukabiliana na viwango vya kawaida vya chakula. Tumbo imepungua katika hicho kipindi cha mfungo. Njia mwafaka ni *kuanza na matunda na maji ya mboga* (supu)na** kisha uanze kutumia machungwa yenyewe na mboga zenyewe**. Ni vyema kuzingatia mpango mzuri wa chakula ili mwili urudie hali yake. (Unaweza kuufwata mwongozo katika vitabu vilivyoko hapo chini.)**

TAMATI
Yesu alisema tunaweza kufunga wakati ambapo Bwana arusi ametwaliwa *(Luka 5:35)*. Kanisa linangojea kurudi kwa Yesu Kristo, Bwana Arusi. Nabii Yoeli alitangaza mara tatu wakati wa kufunga ili Bwana awarudie watu Wake. Ahadi ya kumwaga Roho Wake tunapotii na kufunga na kuomboleza mbele za Mungu. Yesu alianza huduma Yake kwa kufunga. Ni jinsi gani tunahitaji "kutesa nafsi zetu"?

Vitabu Unavyoshauriwa Kusoma.
Prince, Derek, Fasting, (Whitaker House, Springdale PA,1986)

Towns, Elmer.L, Fasting for Spiritual Break Through, (Regal Books, California, 1996)

Wallis, Arthur, God's Chosen Fast, (Kingsway Publications, Ltd. Sussex, 1968)

KUOMBA KATIKA ROHO

Juda 20-21: *"Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu; jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele".*

Kuomba katika Roho ni nini?
Ni kuomba nje ya nia yetu? Ama ni kuomba kutoka kwaroho yetu? Je! Kuna tofauti?

Biblia ina mengi ya kusema juu ya jambo hili na inaonekana kuwa gumu katika kuelewa. Hakuna shaka Mungu anasisitiza mtu na kazi ya Roho Mtakatifu nyakati zetu katika Kanisa Lake. Msingi wetu wa kumjua Roho Mtakatifu na kuelewa kazi Yake hapa duniani, ni sisi tuelewe:
i. sehemu tatu za mtu wa asili
ii. kuzaliwa kwa mtu mara ya pili na kuingia katika ufalme wa Mungu,
iii. kuendelea kujua utofauti kati ya nafsi na Roho.

1Thess.5:23: *"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo. ".* Huu mstari unawasilisha sehemu tatu za mtu. Hitilafu hutokea wakati wa kuelewa tofauti katia ya nafsi na roho.

MWILI
Ni jambo la kuhimiza kujua kuwa Mungu anataka tuhifadhiwe kikamilifu hata miili yetu. ***(Rum.8:23, Fil.3:21).***

NAFSI NA ROHO

Ebr.4:12: *"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho.....,tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo".*
Ni Mungu katika Neno Lake hukawanya nafsi kutoka kwa roho. Kabla mtu hajazaliwa mara ya pili ama kwa Roho ***(Yoh.3:3,5)*** anakuwa *"mfu kwa sababu ya makosa na dhambi"****(Efe.2:1)***. *"Mungu ni Roho; na wamwabuduo imewapasa kumuabudu katika roho na kweli"* ***Yoh.4:24***. Ndiposa lazima tuzaliwe mara ya pili kwa Roho ***(Yoh.3:3,5)***.

ROHO NA NAFSI
Katika aya za ufunguzi za maneno ya unabii ya Mariamu katika ***Luka.1:46-55***, anasema, *"Moyo wangu wamwadhimisha (yamuinua) Bwana, na roho yangu imemfurahia Mungu, mwokozi wangu".* Hapa Mariamu kwa njia ya unabii anatoa utofauti katika kazi ya nafsi na roho. Nafsi yangu inajifunza kuhusu Mungu na kwa hivyo naweza kumsifu na kumuinua kwa maneno ambayo naweza kunena kutoka kwa nafsi yangu.
Roho yangu inamshudia Mungu katika Roho, roho kwa Roho. Roho yangu inafurahia uzima wa Mungu uliomo ndani. Ibada ni ya roho: roho yangu inaitikia Mungu Roho Mtakatifu katika mawasiliano ya rohoni.

NAFSI NA ROHO
Zakaria, baba wa Yohana Mbatizaji, anadhihirisha utofauti katika njia nyingine. Wakati Zakaria alipokutana na Gabrieli, hakunena kutoka kwa roho wake lakini kutoka kwa nafsi yake katika ulimwengu wa kimwili, na kwa hivyo, hangeweza kusadiki ujumbe wa Gabrieli ***(Luka.1:5-22)***. Baadaye katika ***a.67***, maandiko yanasema Zakaria alijazwa Roho Mtakatifu na akatabiri, akisema ... Sasa mawasiliano yake ni tofauti sana, maana

yanatoka mahali tofauti. Awali hangeweza kunena kutoka kwa nia (ambayo ndiyo msingi wa mawazo yote), sasa ananena kutoka kwa Roho aliye ndani ya roho yake, *"tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni"**(1Kor.2:13b).***

MAISHA KATIKA ROHO YANAKUA

Andiko linaweka wazi kwamba maisha katika roho yanaanza na kuzaliwa mara ya pili-mbegu inapandwa ***(1 Pet.1:23)***- halafu inakua kama uhai ndani ukilishwa na kutunzwa. Kuna mengi ambayo yanaweza kusemwa juu ya kukua katika Roho lakini inatosha kwa sasa kuwaleta katika ***1Pet.2:1*** ambapo Petro anatwambia *"tamanini maziwa ya neno"*, na kisha katika ***Ebr.5:12-14***, ambapo mtume anatuhimiza tukue na tuanze kupokea *"chakula kigumu"*. Jaribio la kukua huku ni kuweza kufundisha *"mafundisho ya kwanza ya Kristo "* ya maisha ya Kikristo kwa wengine.

Mara mtu anapozaliwa mara ya pili, na kuanza kutafuta maisha ya rohoni, nafsi inalishwa na kuanza kuongozwa na Roho Mtakatifu na kwa kuendelea kujua Neno la Mungu. Roho ya mwanadamu sasa inahuishwa kwa ajili ya Mungu na roho inakua kutoka kwa mbegu hadi kuwa mtu mkamilifu katika Roho. Kuomba katika Roho ni kuomba kutoka kwa, na katika ufahamu wa mapenzi ya Mungu.
Ni kuomba katika uhai wa ukweli wa Roho. ***Rum.8:14*** *"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu".*
Kumbuka funzo kutoka kwa ***Yohana 15***: Neno la`Rhema' la Yesu likikaa ndani yetu ni msingi wa maombi kujibiwa. Huku kukaa ni huduma ya Roho Mtakatifu.

KUOMBA KATIKA ROHO NI MAOMBI YANAYOONGOZWA NA ROHO

Roho wa Mungu huchunguza yote hata mafumbo ya Mungu na kuwafunulia watakatifu. ***(1Kor.2:10-16)*** Ni kwa njia ya Roho Mtakatifu tunakuja kumfahamu Mungu (kuzaliwa upya) na kupitia kwake ufahamu wa kweli na maarifa ya Mungu yanajulikana kwetu. Ndiposa Paulo anatuombea katika ***Efe.1:17-19***, kwamba *"macho ya ufahamu wetu yatiwe nuru"*, na Mungu awape *"roho wa hekima na ufunuo katika kumjua Yeye."* Hatumjui ama hatumwelewi Mungu katika nia zetu za kibinadamu ila kwa Roho *"atokaye kwa Mungu"* ***(1Kor.2:12).***

Kuomba katika Roho basi ni maombi ambayo chanzo chake ni Roho Mtakatifu.

Anapeana ufunuo na ufahamu, mwongozo na uwezo wa kuomba.

Kipawa cha Kunena Kwa Lugha Mpya:

Kupitia kwa kipawa cha kunena kwa lugha mpya, Roho Mtakatifu anampa mtu rohoni lugha ya Roho ambayo hunena (huomba) moja kwa moja kwa Mungu Mwenyezi ***(1Kor.14:2).*** Hiki kipawa husaidia kuomba katika Roho kwa njia kuu mtu anavyowezeshwa kuomba katika lugha ya Roho, kujijenga maisha yako mwenyewe ya kiroho na mlipuko, kumwezesha mtu kutembea katika nia ya Roho moja kwa moja. ***(1Kor.2:16b)***.
Kama vile Paulo anavyoelezea katika ***1Kor.14:13-19***, tunaweza kuimba na kuomba Mungu kwa njia inayofaa katika roho zetu, na hata zaidi wakati ambapo ufahamu unapokuja katika nia zetu tunaomba katika ufahamu huo na katika roho zetu.

Kujijenga:
"Mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana'(Juda20): "anayenena kwa lugha mpya anajijenga mwenyewe" (1Kor.14:4). Paulo anamshukuru Mungu kwamba ananena kwa

lugha kutuliko sisi sote, lakini faraghani, sio kanisani. *(a.18-19)* Wakati ninapoomba katika lugha, ninaomba kwa roho yangu kwa njia ya kipawa cha lugha ambacho Bwana alinipa aliponibatiza katika (na) Roho Mtakatifu. Ninaomba katika Roho. Sineni na mwili (kwa ujumla) lakini kwa Mungu, nikinena siri ambazo Mungu tu ndiye anayezifahamu. Katika *a.28*, Paulo anasema kijinenea na kumnenea Mungu katika lugha.

Kunena katika Roho:
Katika ***Matendo 4:8***, Petro ananena katika kutetea muujiza ulikuwa umafanyika. *Akiwa amejazwa Roho Mtakatifu na kusema...*" Wakati watakatifu walipoomba pamoja katika ***Matendo 4:24-31***, hakika walikuwa wakiomba katika Roho, na matokeo yakawa kwamba wote wakajazwa na Roho Mtakatifu.

Kuomba katika Roho hakuwezi kulinganishwa na kunena kwa lugha tu lakini kunahuzisha njia yo yote ambayo Roho anaongoza. Wakati uo huo, tusifanye "kawaida" kuomba katika Roho kwamba ni kwa kila maombi. Mara nyingi tunajaribiwa kuomba tu katika ufahamu, wa nia zetu.

Kanuni ya kuomba katika Roho katita Kikundi:

Tumeshiriki kuhusu kuomba kulingana na maandiko na kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa katika maandiko. Kuna kanuni katika Biblia ambazo zaweza kutumiwa katika kuomba katika Roho, katika kikundi. Kama tu Paulo anavyosema katika ***1Kor.14:29*** *"acha manabii wawili ama watatu wanene, na wengine wapambanue"*, kwa hivyo katika maombi ya ushirika, wawili au watatu waombe katika makubaliano kwa kitu Fulani, wakithibitisha nia ya Roho kikamilifu, na wengine wapambanue. Kisha songa mbele kwa jambo lingine kama vile Roho anavyoongoza.
Wakati mwingine tunaweza kwenda kwa haraka; wakati mwingine tunahitaji kungojea, kusikiza na kutimiza ombi katika Roho.

WANAWALI WATANO WENYE BUSARA.
Mfano wa wanawali kumi ni fundisho lililowazi kuhusu hitaji la kujazwa Roho Mtakatifu, usikose mafuta, wakati wakurudi Kwake kunapokaribia. Mafuta yanawakilisha Roho Mtakatifu. Tunahitaji mafuta mengi wakati wa kurudi mara ya pili kunapokaribia. Natuendelee kuomba katika Roho tunapongojea rehema za Bwana wetu Yesu Kristo. Tumeambiwa tuombe bila kukoma. Inawezekana ukaomba kwa lugha yako, mara nyingi, hata wakati nia yako iko kwa mambo mengine. Tunaweza kuomba kwa lugha kimoyomoyo, roho yetu ikiomba katika lugha ya maombi. Maisha yetu ya maombi yanapokua na maisha katika Roho yanaendelea kukua siku baada ya siku, tunaweza kujua wakati ambapo roho zetu zinaomba, tukiliitia jina la Bwana, wakati nia zetu zimetulia juu ya swala lililoko mbele zetu katika ulimwengu wa asili.